

## **WIMBO WA CHUO**

## **A.D. Mligo**

1. Ee Mungu wetu, uwe mwanzo na mwisho wa yote. Tunayofanya, tunayosema. Kwa upendo wako kwetu sisi wanadamu. (Utuongoze tupate mafanikio katika shughuli zetu) x 2
2. Tunakuomba Mungu, bariki chuo chetu Stella Maris. Kiwe ni mwanga wa matumaini, kwa jamii na maendeleo ya binadamu mzima. (Utuongoze tupate mafanikio katika shughuli zetu) x 2
3. Tujalie Baraka, wanafunzi wote wa chuo. Tuwe na maadili, pia wenyе bidii, katika masomo na katika fani za michezo. (Utuongoze tupate mafanikio katika shughuli zetu) x 2
4. Ee Mungu uwalinde, viongozi na wafanyakazi. Wawe na Umoja mshikamano, kuleta mafanikio ya chuo chetu. (Utuongoze tupate mafanikio katika shughuli zetu) x 2
5. Tunaiombea nchi yetu, amani na upendo vitawale. Mshikamano uaminifu, utawala bora, utu kwa kila binadamu. (Utuongoze tupate mafanikio katika shughuli zetu) x 2